# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

70 Barabara ya Chukwani, Buyu,
70490 Mjini Magharibi,
S.L.P 902 Chukwani,
Zanzibar, Tanzania

Simu: +255 24 224 2000
Nukushi: +255 24 2242000
info@zanzibarassembly.go.tz

www.zanzibarassembly.go.tz

## HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA BAJETI KUHUSU MAPENDEKEZO YA MPANGO WA MAENDELEO NA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

### UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** Shukrani za dhati zinamstahikia Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa neema zake zisizohesabika kwa kutujaalia uhai na afya njema tukaweza kutimiza wajibu wetu wa kuwawakilisha wananchi wa Zanzibar. Kwa rehema zake, leo tumekusanyika katika Baraza hili Tukufu tukiwa katika hali ya usalama, amani na utulivu ili kujadili masuala muhimu yanayohusu maendeleo na ujenzi wa nchi yetu. Tunamuomba Mwenyezi Mungu aendelee kuilinda na kudumisha mazingira ya amani, umoja na mshikamano, ambayo ni msingi muhimu wa maendeleo endelevu ya nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba nichukue fursa hii pia kukushukuru wewe Spika wa Baraza la Wawakilishi, Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid kwa namna unavyosimamia na kuendesha vikao vya Baraza letu Tukufu kwa weledi, umakini na ufanisi mkubwa. Ni dhahiri kwamba uongozi wako thabiti katika kuendesha shughuli za Baraza umekuwa chachu ya kulifanya Baraza hili kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na utulivu unaostahili. Aidha, natoa shukrani za dhati kwa wasaidizi wako, Naibu Spika Mheshimiwa Mwanaasha Khamis Juma, pamoja na Wenyeviti wa Baraza ambao mchango wao umeendelea kuimarisha ufanisi wa uendeshaji wa shughuli za Baraza letu.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kutumia fursa hii adhimu kupitia Baraza lako Tukufu kumshukuru na kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, kwa uongozi wake wa busara, uadilifu na maono ya kimkakati ambao umeiwezesha nchi yetu kuendelea

kudumisha amani na utulivu, sambamba na kuimarisha utekelezaji wa mipango ya maendeleo na bajeti za Serikali. Jitihada zake zinaonekana wazi kupitia utekelezaji wa miradi ya maendeleo na uimarishaji wa huduma kwa wananchi.

**Mheshimiwa Spika,** Katika kuendeleza usimamizi wa Serikali, Mheshimiwa Rais wa Zanzibar anapata mashirikiano ya karibu kutoka kwa Msaidizi wake Mkuu, Makamo wa Pili wa Rais wa Zanzibar Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla, ambaye ninampongeza kwa mchango wake muhimu wa ushauri na uratibu unaosaidia kuhakikisha utekelezaji mipango ya maendeleo na bajeti za Serikali unafanyika kwa ufanisi mkubwa.

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya utangulizi na shukurani hizo, naomba sasa kuanza kuwasilisha Hotuba hii ya Maoni ya Kamati ya Bajeti kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

## TATHMINI YA HALI YA UCHUMI WA ZANZIBAR KWA MWAKA 2025

### Mwenendo wa Uchumi

**Mheshimiwa Spika,** Takwimu zinaonesha kuwa, uchumi wa Zanzibar umeendelea kuimarika katika mwaka 2025, ambapo kasi ya ukuaji imefikia asilimia 7.0 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 7.1 mwaka 2024. Ukuaji huo umechangiwa kwa kiasi kikubwa na kuimarika kwa sekta mbalimbali, hususan mapato ya kodi za bidhaa pamoja na ongezeko la idadi ya watalii wanaoingia nchini waliofikia 917,167 mwaka 2025 kutoka watalii 736,755 mwaka 2024. Kamati inaipongeza Serikali kwa mafanikio haya muhimu ya kiuchumi, na inaishauri kuendelea kuimarisha usimamizi wa ukuaji huu ili uwe na manufaa ya moja kwa moja kwa wananchi kwa kuongezeka kwa kipato cha mtu mmoja mmoja, upatikanaji wa fursa zaidi za ajira, kupungua kwa kiwango cha umaskini na hatimaye kuongezeka kwa mapato ya Serikali kwa ujumla.

### Mwenendo wa Mfumko wa Bei

**Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2025, mfumuko wa bei umepungua na kufikia wastani wa asilimia 4.1 ikilinganishwa na asilimia 5.1 mwaka 2024, hali iliyochangiwa kwa kiasi kikubwa na kupungua kwa bei za baadhi ya bidhaa za chakula pamoja na hatua mbalimbali zilizochukuliwa na Serikali kudhibiti mfumko huo na kuhakikisha upatikanaji wa bidhaa na huduma kwa wananchi. Kamati

inaipongeza Serikali kwa mafanikio hayo ya kudhibiti mfumko wa bei ambayo yameleta nafuu kwa wananchi na kupunguza gharama za maisha kwa wananchi, kuwawezesha kufanya manunuzi ya mahitaji yao muhimu kwa urahisi zaidi na hivyo kuimarisha ustawi wa kiuchumi wa jamii kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** Sambamba na hilo, Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuimarisha mikakati ya kudhibiti mabadiliko ya bei kwa kuhakikisha upatikanaji endelevu wa bidhaa muhimu, hususan chakula, pamoja na kuimarisha usimamizi wa masoko na mifumo ya usambazaji ili kuzuia mianya ya ongezeko holela la bei. Aidha, Serikali iendelee kuchukua hatua za kisera zitakazowezesha utulivu wa bei kwa muda mrefu ili wananchi waendelee kunufaika na hali ya uchumi ulio imara.

## Hali ya Ajira Nchini

**Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2024/2025, ajira mpya zilizosajiliwa Serikalini, mashirika ya umma na sekta binafsi zimeongezeka na kufikia jumla ya ajira 85,182, ikilinganishwa na ajira 83,430 zilizorekodiwa katika mwaka 2023/2024. Kamati inaipongeza Serikali kwa mafanikio haya ya kuongeza fursa za ajira ambazo zimewezesha wananchi kupata kipato cha uhakika cha kukidhi mahitaji yao ya msingi, ikiwemo chakula, mavazi na malazi. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuimarisha mazingira rafiki ya uwekezaji na biashara ili kuvutia miradi zaidi itakayoongeza ajira zenye tija, hususan kwa vijana na wanawake.

**Mheshimiwa Spika,** Vilevile, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa katika mikataba ya uanzishaji wa miradi ya maendeleo na uwekezaji, kipengele cha ajira kwa wazawa kinajumuishwa rasmi na kuwekewa masharti bayana ya utekelezaji wake. Hatua hiyo itawezesha wananchi wazawa kunufaika kikamilifu na fursa za ajira zinazozalishwa, sambamba na kuongeza uwajibikaji wa wawekezaji katika kuchangia maendeleo ya wananchi kwa ujumla.

## Uingiaji wa Watalii

**Mheshimiwa Spika,** Sekta ya utalii imeendelea kukua kwa kasi na kuchangia kwa kiasi kikubwa katika Pato la Taifa, ikiwa ni takribani asilimia 30. Katika mwaka 2025, idadi ya watalii imeongezeka na kufikia takribani 917,167 ikilinganishwa na 736,755 mwaka 2024, hali iliyochangia pia kuimarika kwa mapato ya sekta hii. Kamati inaipongeza Serikali kwa mafanikio haya ambayo yamechochea ongezeko la fursa

za ajira, uwekezaji katika miundombinu na kukuza uchumi kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa ukuaji wa sekta ya utalii unakwenda sambamba na ulinzi wa ajira kwa wazawa kwa kuweka mifumo thabiti ya udhibiti wa ajira zinazopaswa kufanywa na wazawa. Aidha, Serikali ihakikishe kuwa ukuaji wa sekta hii unalinda na kuendeleza utamaduni wa nchi yetu kwani utasaidia vijana wetu katika kufuata mila na silka za Kizanzibari na kutokuiga mila za kigeni. Sambamba na hilo, Serikali ihakikishe kwamba shughuli za utalii haziathiri mazingira na rasilimali asilia ambazo ni msingi muhimu wa uendelevu wa sekta hii kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

### Akiba ya Fedha za Kigeni

**Mheshimiwa Spika,** Serikali inaendelea na jukumu la kuhifadhi akiba ya fedha za kigeni ili kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi. Katika kipindi cha mwaka 2024/2025, akiba hiyo imeongezeka na kufikia takribani Dola za Marekani bilioni 6.2, ikilinganishwa na Dola za Marekani bilioni 5.3 katika mwaka 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa mafanikio haya ambayo yameimarisha uwezo wa nchi kugharamia uagizaji wa bidhaa na huduma muhimu kutoka nje ya nchi pamoja na kuimarisha uthabiti wa uchumi. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuimarisha mikakati ya kuongeza uzalishaji wa ndani na mauzo ya nje ya bidhaa na huduma ili kupunguza utegemezi wa uagizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi, sambamba na kuhakikisha matumizi bora ya akiba ya fedha za kigeni ili kulinda uthabiti wa uchumi wa nchi kwa muda mrefu.

## TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

**Mheshimiwa Spika,** Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2025/2026 ulilenga kutekeleza programu 41 na miradi 56 ya maendeleo, ambapo Serikali ilipanga kutumia jumla ya TZS 4,539.64 bilioni, ikijumuisha TZS 3,231.40 bilioni kutoka Serikalini na TZS 1,308.24 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Hadi kufikia Machi 2026, utekelezaji wa miradi ya maendeleo umefikia TZS 1,769.27 bilioni sawa na asilimia 65 ya lengo la kipindi hicho, ambapo TZS 1,414.53 bilioni zilitokana na

Serikali na TZS 354.74 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo, hali inayoonesha kuwa kiwango cha utekelezaji bado ni kidogo ukilinganisha na makadirio ya mwaka na hivyo kuna haja ya kuongeza kasi ya utekelezaji ili kufikia malengo yaliyopangwa kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** Ili kuimarisha utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo na kuhakikisha miradi yote inatekelezwa kwa ufanisi, kwa wakati na kwa kuzingatia vipaumbele vilivyowekwa, Kamati inaishauri Serikali kuimarisha mifumo ya ufuatiliaji na tathmini ya miradi, kuongeza juhudi za ukusanyaji wa mapato ya ndani, pamoja na kuimarisha ushirikiano na Washirika wa Maendeleo ili kuhakikisha upatikanaji wa fedha kwa wakati. Vilevile, Serikali ihakikishe kunakuwa na mgawanyo wenye uwiano mzuri wa fedha za miradi kwa kuendelea kuipa kipaumbele miradi ya kimkakati yenye manufaa ya moja kwa moja kwa wananchi, na kuimarisha uratibu na tathmini za mara kwa mara ili kuongeza ufanisi na tija katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kuimarisha uwazi na uwajibikaji katika usimamizi wa miradi ya maendeleo ili kupunguza ucheleweshaji na kuongeza thamani ya fedha. Pia, Serikali iendelee kuimarisha uwezo wa taasisi husika katika usimamizi wa miradi, pamoja na kuhakikisha taarifa za utekelezaji zinapatikana kwa wakati ili kuwezesha maamuzi sahihi na ya haraka katika ngazi zote za utekelezaji.

## TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

### Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Kipindi cha Julai – Machi 2025/2026

**Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha miezi tisa ya mwaka wa fedha 2025/2026, Serikali ilikadiria kukusanya jumla ya TZS 3,621.61 bilioni kutoka vyanzo mbalimbali vya mapato ya ndani na nje, ambapo hadi kufikia Machi 2026 mapato halisi yalifikia TZS 3,633.87 bilioni, sawa na asilimia 100.34 ya lengo la kipindi hicho. Kamati inaipongeza Serikali kwa mafanikio haya ya kuridhisha katika ukusanyaji wa mapato. Hata hivyo, inaishauri Serikali kuimarisha zaidi usimamizi wa mapato ya Serikali za Mitaa na taasisi zinazojitegemea kwa kuimarisha mifumo ya ukusanyaji na udhibiti wa vyanzo vyake, ili kuondoa changamoto zinazoendelea kujitokeza katika maeneo

hayo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia inaishauri Serikali kufanya tathmini ya kina ya mapato yasiyo ya kodi ili kubaini njia bora zaidi za ukadiriaji na ukusanyaji wake, kwa kuwa mapato hayo bado hayatoi mchango unaotarajiwa katika baadhi ya Wizara na taasisi za Serikali. Vilevile, Kamati inaishauri Serikali kuimarisha matumizi ya mifumo ya kidijitali katika ukusanyaji wa mapato ili kuongeza uwazi, kupunguza mianya ya upotevu wa mapato na kuongeza ufanisi wa ukusanyaji.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa matumizi, katika kipindi cha miezi tisa ya mwaka wa fedha 2025/2026, Serikali ilikadiria kutumia TZS 3,406.4 bilioni, ambapo hadi kufikia Machi 2026 matumizi halisi yalifikia TZS 3,416.3 bilioni, sawa na asilimia 100.29 ya makadirio ya kipindi hicho. Kamati inaisisitiza Serikali kuendelea kuimarisha nidhamu ya matumizi ya fedha za umma kwa kuhakikisha yanazingatia kikamilifu makadirio ya bajeti ya kipindi husika. Vilevile, Serikali iendelee kuimarisha mifumo ya ufuatiliaji na udhibiti wa matumizi ili kuhakikisha uwiano kati ya mapato na matumizi unazingatiwa, pamoja na kuongeza uwajibikaji katika ngazi zote za utekelezaji wa bajeti.

### Utekelezaji wa Mapendekezo ya Hatua za Kuimarisha Mapato kwa Kipindi cha Julai 2025 – Machi 2026

**Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai hadi Machi 2025/2026, Serikali ilitekeleza hatua mbalimbali za kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa lengo la kuongeza uwezo wa kugharamia shughuli za maendeleo na huduma za kijamii. Hatua hizo zilijumuisha marekebisho ya sheria na uimarishaji wa usimamizi wa kodi, hususan katika kukuza uzalishaji wa viwanda vya ndani, kuimarisha udhibiti wa forodha, kuimarisha usimamizi wa vyombo vya moto, kuimarisha huduma jumuishi za kifedha na kuongeza ufanisi wa utawala wa kodi kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali imebainisha kuwa miongoni mwa hatua zilizo chukuliwa ni marekebisho Sheria ya Ushuru wa Bidhaa Na. 8 ya mwaka 2017 ambapo ushuru wa uingizaji wa kuku na samaki uliongezwa hadi TZS 1,000 kutoka TZS 300, hatua ambayo imechangia kukusanya takribani TZS 3.922 bilioni.

**Mheshimiwa Spika,** Licha ya mafanikio hayo ya kuongeza mapato, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha hatua hizi pia zinakwenda sambamba na kuimarisha uzalishaji

wa ndani ili kupunguza utegemezi wa uagizaji wa bidhaa hizo kutoka nje. Vilevile, Kamati inaishauri Serikali kutoa tathmini na ufafanuzi wa kina unaoonesha namna hatua hizo zilivyosaidia kupunguza uingizaji wa bidhaa hizo na kuongeza uzalishaji wa ndani.

## Uchambuzi wa Hali ya Deni la Taifa

**Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi 2026, deni la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar limefikia TZS 3,001.63 bilioni, likijumuisha deni la ndani la TZS 2,987.03 bilioni na deni la nje la TZS 14.6 bilioni, ambapo kwa ujumla uwiano wa deni hilo kwa Pato la Taifa la TZS 6,572.6 bilioni ni asilimia 40.63.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kuimarisha zaidi ukusanyaji wa mapato ya ndani ili kupunguza utegemezi wa mikopo na misaada kutoka nje, pamoja na kuongeza ufanisi katika usimamizi wa mapato ya Serikali. Vilevile, Serikali ihakikishe mikopo hiyo inalipwa kwa wakati ili kuepuka ongezeko la gharama za riba na kulinda uendelevu wa taasisi za kifedha. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa kasi ya ongezeko la deni inaendana na uwezo wa kulihudumia kwa kuimarisha mapato na usimamizi wa matumizi, na kuweka mikakati madhubuti ya kuhakikisha uwiano wa deni kwa Pato la Taifa unadhibitiwa chini ya kikomo kinachokubalika cha asilimia 55 cha uhimilivu wa deni la nchi.

## Dhamana kwa Taasisi za Serikali

**Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi 2026, Serikali imetoa dhamana za Serikali zenye thamani ya TZS 300.345 bilioni kwa taasisi mbalimbali za umma. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua ya kuzisaidia taasisi zake kupitia dhamana hizo ili kuwezesha upatikanaji wa mikopo kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake. Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuweka bayana masharti na vigezo kabla ya kutoa dhamana hizo, ikiwemo kuhakikisha mikopo hiyo inalipwa kwa wakati, na kwamba fedha zinazopatikana zinatumika kwa tija katika uwekezaji na kuimarisha utoaji wa huduma kwa wananchi pamoja na uendelevu wa taasisi husika.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande mwengine, Kamati inaishauri Serikali kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji wa dhamana zote zinazotolewa ili kuhakikisha hatari za kifedha zinadhibitiwa mapema. Vilevile, Serikali ihakikishe kunakuwa na tathmini ya kina ya

uwezo wa taasisi husika kabla ya kuidhinisha dhamana, ili kuepusha mzigo usio wa lazima kwa Serikali na kulinda uhimilivu wa madeni ya umma kwa muda mrefu.

### Misamaha ya Kodi

**Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Serikali ilipokea maombi 474 ya misamaha ya kodi kutoka taasisi za umma na binafsi, ikiwa ni ongezeko kubwa ukilinganisha na maombi 294 yaliyopokelewa katika mwaka 2024/2025. Kamati inaishauri Serikali kupitia upya masharti ya utoaji wa misamaha ya kodi ili kuhakikisha inatolewa kwa uangalifu na kwa vipengele mahsusi vya miradi husika badala ya kutoa msamaha wa jumla. Aidha, miradi inayopatiwa misamaha hiyo ihakikishwe inaleta manufaa ya kiuchumi na kijamii kwa nchi, kwa kuzingatia kuwa misamaha ya kodi hupunguza wigo wa mapato ya Serikali. Vilevile, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha wawekezaji wa ndani pia wananufaika na misamaha hiyo kwa uwiano stahiki ili kuchochea ukuaji wa sekta binafsi na kuimarisha uwekezaji wa ndani.

### Matarajio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Kipindi cha Julai – Juni Mwaka wa Fedha 2025/2026

**Mheshimiwa Spika**, Hadi kufikia mwisho wa mwaka wa fedha 2025/2026, Serikali inatarajia kukusanya jumla ya TZS 6,386.88 bilioni, sawa na asilimia 91 ya lengo la TZS 6,982.08 bilioni, ikiwa ni ongezeko la takribani asilimia 36 ikilinganishwa na makusanyo ya mwaka 2024/2025. Kamati inaipongeza Serikali kwa mwenendo huo chanya wa ongezeko la makusanyo ya mapato. Hata hivyo, inaishauri Serikali kuimarisha zaidi udhibiti wa mianya ya upotevu wa mapato kwa kuunganisha kikamilifu mifumo ya ukusanyaji ili kuhakikisha uwazi, ufuatiliaji na udhibiti wa miamala yote ya mapato kutoka vyanzo vyote vya Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Sambamba na hilo, Kamati inaishauri Serikali kuimarisha matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato ili kupunguza mianya ya upotevu na kuongeza ufanisi.

## TATHMINI YA MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI WA ZANZIBAR KWA MWAKA 2026

**Mheshimiwa Spika,** Takwimu zinaonesha kuwa uchumi wa Zanzibar unatarajiwa

kukua kwa asilimia 7.5 mwaka 2026, ukichangiwa na kuongezeka kwa watalii wataofikia takribani milioni 1.0, utekelezaji wa miradi mikubwa ya kimkakati ya miundombinu na huduma za jamii, kuimarika kwa mazingira ya biashara na uwekezaji, pamoja na kuongezeka kwa mchango wa sekta binafsi na sekta ya uchumi wa buluu. Vilevile, uthabiti wa bei na kuimarika kwa mapato ya ndani kunatarajiwa kuchangia kwa kiasi kikubwa mwenendo huo wa ukuaji.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua madhubuti zinazolenga kuimarisha misingi ya uchumi na kuchochea shughuli zinazogusa maisha ya wananchi moja kwa moja, hususan katika kuongeza fursa za ajira, uwekezaji na kipato cha kaya. Aidha, Kamati inaona kuwa mwelekeo huu wa uchumi ukisimamiwa kwa ufanisi utachochea zaidi ustawi wa wananchi na kuimarisha ushindani wa Zanzibar katika uchumi wa kikanda na kimataifa. Kwa ujumla, matarajio ya ukuaji huu yanajengwa juu ya kuimarika kwa sekta za uzalishaji, utalii, miundombinu na huduma za kijamii, ambazo kwa pamoja zinatoa mwelekeo chanya wa maendeleo endelevu ya nchi yetu.

## TATHMINI YA MAPENDEKEZO YA MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

**Mheshimiwa Spika,** Kupitia Mpango wa Maendeleo wa mwaka wa fedha 2026/2027, Serikali imeelekeza juhudi zake katika kuimarisha ukuaji wa uchumi, kuinua ustawi wa wananchi na kuimarisha utoaji wa huduma za kijamii. Mpango huu umejikita katika utekelezaji wa programu na miradi ya kimkakati inayolenga kuchochea maendeleo endelevu, kuongeza fursa za ajira, kuimarisha mazingira ya uwekezaji na kuimarisha huduma muhimu kwa wananchi.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2026/2027 Serikali imepanga kutumia jumla ya TZS 5,281.03 bilioni kwa ajili ya utekelezaji wa programu 42 na miradi 64 ya maendeleo, ambapo TZS 3,920.59 bilioni zitaelekezwa katika miradi ya kimkakati na TZS 1,360.44 bilioni kwa miradi mingine inayoendelea pamoja na ile ya mashirikiano na Washirika wa Maendeleo. Aidha, utekelezaji huo unatarajiwa kuchochea mageuzi katika sekta za Uchumi wa Buluu, kilimo cha biashara, miundombinu, nishati, maji, TEHAMA, afya, elimu na utawala bora, kwa lengo la kuongeza ufanisi wa huduma na ustawi wa wananchi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuweka msisitizo katika miradi ya kimkakati yenye mchango wa moja kwa moja katika maisha ya wananchi na ukuaji wa uchumi wa nchi yetu. Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuweka mkazo katika miradi yenye mchango wa moja kwa moja katika kukuza uchumi, kuongeza ajira, kuimarisha huduma za kijamii na kuimarisha ustahimilivu wa nchi dhidi ya changamoto za kiuchumi na mazingira, ili dhamira ya kuleta maendeleo endelevu na ustawi wa wananchi iweze kufikiwa kwa kiwango kinachotarajiwa.

**Mheshimiwa Spika,** Ili kufanikisha utekelezaji wenye tija wa Mpango wa Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2026/2027 na kuhakikisha kuwa malengo yaliyowekwa yanafikiwa kwa ufanisi unaotarajiwa, sambamba na kuimarisha ukuaji wa uchumi na ustawi wa wananchi, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa upatikanaji wa fedha za maendeleo unakuwa wa uhakika na wa wakati ili miradi yote iliyopangwa iweze kutekelezwa kwa ufanisi na kukamilika kwa mujibu wa malengo yaliyowekwa. Aidha, Serikali iongeze juhudi katika kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani ili kupunguza utegemezi mkubwa wa fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo sambamba na kuimarisha mifumo ya ufuatiliaji na tathmini ya miradi ili kuhakikisha thamani ya fedha inapatikana katika utekelezaji wa miradi hiyo.

## TATHMINI YA MAPENDEKEZO YA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Serikali inatarajia kukusanya jumla ya TZS 8,525.85 bilioni, ikiwa ni ongezeko la asilimia 22.32 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2025/2026. Aidha, mapato ya ndani yanatarajiwa kufikia TZS 7,011.454 bilioni, sawa na ongezeko la asilimia 26.62 kutoka makadirio ya mwaka uliopita. Mwelekeo huu unaonesha dhamira ya Serikali ya kuimarisha uwezo wa ndani wa kugharamia shughuli za maendeleo na utoaji wa huduma kwa wananchi, sambamba na kuongeza mchango wa vyanzo vya mapato vya ndani katika utekelezaji wa bajeti ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Miongoni mwa mikakati iliyowekwa na Serikali ni kuimarisha mifumo ya ukusanyaji wa mapato na kuhakikisha mapato yote yanakusanywa kupitia mifumo ya kielektroniki. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hiyo muhimu inayolenga kuongeza uwazi, uwajibikaji na ufanisi katika ukusanyaji wa mapato. Hata

hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua za haraka kutatua changamoto zilizopo katika Mfumo wa Zan Malipo unaotumika kama mfumo mkuu wa ukusanyaji wa mapato kwa taasisi za Serikali, ili kuimarisha ufanisi wa mfumo huo na kuondoa changamoto zote zinazoweza kuathiri juhudi za ukusanyaji wa mapato nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) inatarajiwa kukusanya TZS 1,726.66 bilioni, huku Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) - Zanzibar ikitarajiwa kukusanya TZS 1,144.69 bilioni. Aidha, mapato yasiyokuwa ya kodi yanakadiriwa kufikia TZS 351.80 bilioni.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inazipongeza Mamlaka hizo za kikodi kwa juhudi kubwa inazozichukua katika ukusanyaji wa mapato ya Serikali, ambapo kwa miaka kadhaa zimeendelea kufikia na hata kuvuka malengo ya makusanyo, hali inayojenga matumaini ya kufikiwa kwa malengo ya mapato yaliyopangwa kwa mwaka 2026/2027. Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuimarisha zaidi usimamizi na ukusanyaji wa mapato yasiyokuwa ya kodi kwa kuweka mifumo madhubuti ya ufuatiliaji kuanzia katika vyanzo vyake. Aidha, Serikali itafute utaratibu bora wa kuyasimamia mapato hayo ili yaweze kutoa mchango mkubwa zaidi katika kuongeza mapato ya ndani.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Serikali inatarajia kupokea TZS 1,514.396 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo kupitia mikopo na misaada kwa ajili ya kugharamia bajeti na utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kamati inaipongeza Serikali kwa jitihada zake za kuendelea kupunguza utegemezi wa misaada ya nje na kuelekeza zaidi matumizi ya mikopo yenye masharti nafuu kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo. Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuongeza juhudi katika ukusanyaji wa mapato ya ndani na kuendelea kupanua wigo wa vyanzo vya mapato ili kuimarisha uwezo wa nchi kujitegemea kifedha. Hatua hii ni muhimu hasa katika kipindi hiki cha mabadiliko na misukosuko ya kiuchumi na kisiasa duniani ambayo inaweza kuathiri upatikanaji wa fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa matumizi, kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Serikali inakadiria kutumia jumla ya TZS 8,525.85 bilioni, ambapo TZS 5,788.37 bilioni sawa na asilimia 67.9 zitaelekezwa katika shughuli za maendeleo, huku TZS 2,737.48 bilioni sawa na asilimia 32.1 zikitumika kwa kazi za kawaida. Kamati

inaipongeza Serikali kwa kuendelea kutoa kipaumbele kikubwa kwa matumizi ya maendeleo, hususan katika utekelezaji wa miradi mipya ya kimkakati na ile inayoendelea.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia inaishauri Serikali kuimarisha mifumo ya manunuzi ya umma kwa kuhakikisha michakato ya ununuzi inazingatia uwazi, ushindani wa haki na thamani ya fedha. Pia, Serikali ihakikishe taasisi zote zinatumia kikamilifu mifumo ya kielektroniki ya manunuzi ili kupunguza mianya ya ubadhirifu, kuchelewesha taratibu na kuongeza ufanisi katika matumizi ya fedha za umma.

## Mikakati ya Upatikanaji wa Rasilimali Fedha

**Mheshimiwa Spika,** Serikali imeweka mikakati mbalimbali ya kuimarisha upatikanaji wa fedha, ikiwemo kuongeza mapato yasiyo ya kodi kupitia uimarishaji wa usimamizi wa mali za Serikali na kuimarisha ufanisi wa Mashirika ya Umma ili kuongeza gawio na michango kutoka katika taasisi zinazojitegemea. Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuimarisha zaidi mapato yasiyo ya kodi kwa kuweka mikakati mahsusi ya kuongeza ufanisi katika makusanyo ya Wizara na taasisi za Serikali, ambayo kwa muda mrefu yamekuwa yakikabiliwa na changamoto mbalimbali katika utekelezaji wake.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia inaishauri Serikali kuimarisha zaidi utekelezaji wa mikakati ya uhamasishaji wa vyanzo mbadala vya upatikanaji wa fedha kama Sukuk, Green Bond na Blue Bond kwa kuweka mifumo madhubuti ya kitaasisi na kisheria utakaorahisisha uandaaji, uuzaji na usimamizi wa vyanzo hivyo. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kufanya tafiti za kina za soko ili kubaini mahitaji ya wawekezaji wa ndani na nje, na kuhakikisha bidhaa hizo za kifedha zinaundwa kwa muundo unaovutia na unaoendana na hali ya soko. Vilevile, Serikali iendelee kuimarisha elimu kwa umma na kampeni za uhamasishaji ili kuongeza ushiriki wa wananchi katika uwekezaji, sambamba na kuhakikisha uwazi, uaminifu na usimamizi madhubuti wa matumizi ya fedha zitakazopatikana kupitia vyanzo hivyo.

## Vipaumbele vya Bajeti kwa Kuzingatia Sera za Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

**Mheshimiwa Spika,** Kwa ujumla Serikali imetenga TZS 3,797.39 bilioni kwa ajili ya

utekelezaji wa miradi ya kimkakati mipya pamoja na miradi inayoendelea, ikiwa ni hatua muhimu katika kuimarisha utekelezaji wa ajenda ya maendeleo ya nchi yetu. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kuweka kipaumbele katika miradi inayogusa maisha ya wananchi moja kwa moja kupitia sekta mbalimbali kama vile miundombinu, huduma za kijamii, mageuzi ya kiuchumi na utawala bora. Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuimarisha usimamizi na uratibu wa miradi kwa kuhakikisha kipaumbele cha kwanza ni kukamilika kwa miradi iliyoanza kabla ya kuanzisha miradi mipya, ili kuepuka usambazaji mdogo wa fedha na kuchelewesha matokeo yanayotarajiwa. Aidha, Kamati pia inaishauri Serikali iendelee kuimarisha ufuatiliaji wa matumizi na kuhakikisha thamani ya fedha inapatikana.

**Mheshimiwa Spika,** Miongoni mwa vipaumbele vya bajeti ya mwaka 2026/2027 ni utekelezaji wa bajeti inayozingatia jinsia na usawa, ili kuhakikisha rasilimali za nchi zinawanufaisha wananchi wote kwa uwiano mzuri. Kipaumbele hiki pia kilitekelezwa katika bajeti ya mwaka 2025/2026 ambapo Serikali ilitenga TZS 71.93 bilioni kwa wizara nane za mfano kwa ajili ya kuimarisha usawa wa kijinsia na kufanikisha malengo ya kitaifa katika eneo hilo. Katika mwaka 2026/2027, Serikali imetenga TZS 449.80 bilioni kwa ajili ya kuimarisha masuala ya jinsia na usawa katika sekta mbalimbali. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hiyo muhimu na inaishauri Wizara na taasisi husika kuhakikisha fedha hizo zinatumika kikamilifu kwa mujibu wa mipango iliyowekwa ili kufikia malengo yaliyokusudiwa kwa ufanisi.

## HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kumalizia, napenda kutumia nafasi hii kukushukuru kwa kunipa fursa ya kuwasilisha Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Bajeti kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Aidha, ninawapongeza na kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Bajeti kwa ushirikiano wao mkubwa, weledi na kujituma katika kutekeleza majukumu ya Kamati, jambo lililowezesha kufanikisha maandalizi na kukamilika kwa hotuba hii. Kwa kutambua mchango wao muhimu, naomba niwatambue kwa majina yao kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Ali Suleiman Ameir | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Maryam Said Khamis | Makamo Mwenyekiti |

| | | |
|---|---|---|
| 3. | Mhe. Bakar Hamad Bakar | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Farida Amour Mohammed | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Mohammed Ali Salim | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Sulubu Kidongo Amour | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Yussuf Ali Hassan | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika,** Kwa namna ya kipekee, napenda kumshukuru Waziri wa Fedha na Mipango (WFM) Mheshimiwa Dkt. Juma Malik Akil pamoja na Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Hamad Omar Bakar kwa ushirikiano mkubwa waliyoipatia Kamati ya Bajeti katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu yake katika upitishaji wa Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2026/2027 katika ngazi ya Kamati. Aidha, ninatoa shukrani zangu kwa watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Mipango (WFM) pamoja na taasisi zake zote inazozisimamia kwa ushirikiano na ufafanuzi wao uliyoiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika,** Mwisho kabisa, napenda kutoa shukrani maalum kwa Ofisi ya Baraza la Wawakilishi chini ya uongozi wa Katibu wa Baraza, Ndugu Raya Issa Msellem pamoja na watumishi wote wa Baraza kwa ushirikiano wao uliowezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Shukrani maalum nazitoa kwa Kitengo cha Bajeti cha Baraza la Wawakilishi kwa mchango wake mkubwa wa kitaalamu katika kuisaidia Kamati ya Bajeti na Kamati za Kisekta kufanya uchambuzi wa kibajeti, hali iliyoongeza ubora wa mijadala na ushauri kwa Serikali. Aidha, kwa namna ya pekee naipongeza Sekretarieti ya Kamati ya Bajeti kwa uratibu mzuri uliosaidia kufanikisha shughuli za Kamati pamoja na kukamilika kwa hotuba hii. Kwa kuthamini mchango wao mkubwa kwa Kamati, naomba niwatambue kwa majina yao kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Ndg. Asha Said Mohamed | Katibu |
| 2. | Ndg. Maryam Mohammed Othman | Katibu |
| 3. | Ndg. Shaib Fadhil Shaib | Katibu |
| 4. | Ndg. Yussuf Mkamba Mwinyi | Katibu |
| 5. | Ndg. Said Bakar Hamad | Msaidizi wa Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya maelezo hayo, naomba Baraza lako tukufu lijadili na

kuishauri vyema Serikali na hatimae kuidhinisha Mapendekezo haya ya Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027. Nawashukuruni sana kwa kunisikiliza. Naomba kuwasilisha.

Ahsante,

……………….………

Mhe. Ali Suleiman Ameir,
Mwenyekiti,
Kamati ya Bajeti,
Baraza la Wawakilishi,
**Zanzibar.**